

Matatizo yetu yanaanza kichwani

Uk. 4



Walioibiwa laptop watakiwa Polisi

• Ni abiria waliopata
ajali ya ndege Bukoba

Sensa yasahau mahunta

Uk. 6

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Uzembe umulikwe, ukomeshwe

ZIPO kila dalili zinazoonyesha zkurejea kwa kasi kwa uzembe wa baadhi ya watendaji katika ofisi za umma; ndani ya serikali kuu, taasisi na hata mashirika yanayopaswa kuhudumia wananchi kwa ufanisi mkubwa.

Hali hiyo inaonekana katika baadhi ya hospitali zetu, vituo vya Polisi, ofisi za wakuu wa wilaya na mikoa na hata katika ngazi za mawaziri.

Malalamiko ya wananchi wanaokwenda kupata huduma katika ofisi hizo yamekuwa makubwa na yanaongezeka siku hadi siku, huku wanaohitaji huduma wakiteseka kupata haki zao za msingi ndani ya ofisi hizo.

Pambazuko, gazeti la kila wiki linalotolewa bure, linaendelea kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi wanaodai kutotendewa haki katika baadhi ya ofisi za umma wanakokwenda kupata huduma.

Wengi wanalalamika kuhusu baadhi ya watendaji ndani ya ofisi za umma kutokuwepo kwenye sehemu zao za kazi. Hawa wanaelezwa kuchelewa kufika ofisini au hata wakiwamo, wanamaliza muda mwingi wakitumia simu zao za mkononi ama kwa kuwasiliana au pengine “kucheza michezo iliyomo ndani ya simu hizo.”

Kwamba mtumishi wa umma anapokuwa ofisini kwake – badala ya kutumia muda mwingi kuhudumia wateja, yeye anzungumza kwa muda mrefu – kwa simu na watu anaowajua yeye, huku wateja wakisubiri amalize ndipo awahudumie.

Pia wapo baadhi ya watendaji wa ofisi za umma wanaomaliza muda mwingi wa kazi kwa kutazama mambo ya siyofaa kwenye

kompyuta zao, huku wakijifanya kwamba wako “bize.”

Lakini pia wapo wanaotumia muda mrefu zaidi wanapoaga kwenda kunywa chai au kupata chakula cha mchana. Pamoja na kwamba siyo kosa kwenda kupata haki ya chakula, lakini tunaamini upo muda maalum kwa ajili hiyo, na siyo kila wakati mtumishi wa umma anaweza kwenda kula anavyotaka na kumaliza sehemu kubwa ya muda wa kazi anaopaswa kuhudumia wananchi.

Hali hii, katika miaka mitano iliyopita, ilionekana kukoma kwani kulikuwepo kiongozi mfuatiliaji na pengine tunaweza kueleza alikuwa mkali. Rais John Magufuli (sasa marehemu) hakucheka na wazembe ndani ya serikali na hata maeneo mengine.

Kutokana na hulka yake, watendaji wa serikali; wakubwa kwa wadogo kwa dhamana, waliogopa kuzembea kwa aina yoyote. Wengi walifanya kazi, hata kama ni kwa woga, lakini malalamiko ya uzembe kwa watendaji serikalini yalipungua kwa kiasi kikubwa.

Ni katika kipindi hicho, wateja ndani ya ofisi za serikali walionekana kuwa ni wafalme kwelikweli. Hakuna mteja aliyekosa huduma ama kucheleweshwa kwa uzembe.

Sasa basi, pamoja na kuwepo kwa kiongozi wa sasa mwenye upole na kuamini kwa kiasi kikubwa aliowapa dhamana, bado Rais Samia Suluhu Hassan anapaswa kuongeza ukali na kufuatilia kwa ukaribu zaidi watendaji wake ili wananchi wapate huduma stahiki na kuondoa malalamiko.

3



NUKUU



KITU kigumu zaidi katika maisha ni kuamua; unaweza kufanya chochote unachotaka kufanya, unaweza kutenda na kubadili maisha yako kabisa ikiwa tu utaamua kuanza kutenda kile unachokiamini, bila kupima matokeo yake haraka. Wewe fanya na mengine yote yanabaki kuwa matokeo- **Msemu wa Kiswahili.**

Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: pambazuko1@protonmail.com ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Matatizo yetu yanaanza kichwani

Na Thadei ole MUSHI

ETHIOPIA ni nchi yenye idadi ya watu wanaoelezwa kufikia milioni 117. Idadi hii ni mara mbili ya Watanzania wote kwa mujibu matokeo ya sensa ya mwaka huu – 2022 inayotaja kuwepo watu milioni 61.7.

Nchi hiyo ya pembe ya Afrika inapata dola za Marekani milioni 100 kila mwaka kwa kuuza umeme Kenya. Nchi hizo mwezi Oktoba, 2022 zilifunga mkataba wa kuuza na kununua umeme wa megawati 600 kwa miaka 25.

Chanzo kikubwa cha umeme huo ni maji ya Mto Nile ambao unaanzia Ziwa Victoria. Sehemu kubwa ya ziwa hilo iko Tanzania; kwamba asilimia 49 iko Tanzania, Kenya asilimia sita na Uganda asilimia 45.

Sambamba na hilo, Bwawa la Aswan kule Misri linaloyumika kwa matumizi makubwa, ikiwamo hata kuzalisha umeme, chanzo cha maji yake ni kutoka Ziwa Victoria pia linahusika.

Iweje sasa Tanzania imelala tu na kushindwa kutumia maji hayo kuwa chanzo kikubwa cha umeme na shughuli zingine kubwa zenye kuleta mapato zaidi kwa nchi? Au kuna amri ya Mungu kwamba Tanzania itumie maji ya ziwa hilo kwa kuvua sato na sangara tu?

Sijui nani kairoga Tanzania, mbali na maji ya Ziwa Victoria kushindwa kutumika ipasavyo kupunguza umasikini, bado inashangaza nchi yetu kuwa na uhaba wa mafuta ya kula. Kila siku upungufu wa mafuta inakuwa ajenda ya kitaifa wakati tungeweza kuamua tu kuwa nayo mengi zaidi.

Haiieleweki kwanini Tanzania inashindwa kuwa kinara wa kuzalisha na kuuza mafuta ya kula zaidi ya Malaysia kwani hali ya hewa ya nchi hizo inafanana kabisa na kwamba nchi yetu ndiyo ilianza kulima zao hilo na wao wakaja kujifunza na kuchukua mbegu. Wakatuacha “tumelala.”

Maajabu ya nchi hii ni mengi sana,



Ziwa Victoria

mfano mwaka jana Uganda ilisaini mkataba wa kuuza maziwa ya ng'ombe nchini Zambia. Inafikirisha sana – kwamba Uganda na Tanzania ni nchi ipi iko jirani zaidi na Zambia? Kwa nini sisi tusingechukua ‘dili’ hilo la kuwauzia maziwa wakati tuna mifugo lukuki?

Baadaye nikagundua kuwa hata viwanda vyetu vya ndani havina uwezo wa kuuza maziwa ya kutosha , hivyo asilimia kubwa ya maziwa tunayotumia tunaagiza nje, hasa maziwa ya unga.

Uganda kwa mwaka wanazalisha maziwa lita bilioni 2.8; Kenya lita bilioni 3.43 huku Tanzania ikiwa inazalisha lita milioni 470 kwa mwaka. Ajabu sana!

Hivi karibuni, Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollle alisema tatizo kubwa la nchi za Afrika siyo uhaba wa rasilimali, bali ni kutokuheshimu akili kubwa.

Uonevu kwa wanawake ukomeshwe

Na Tryruckia MFINANGA

KILA dakika moja inayopita duniani, mwanamke mmoja hupoteza maisha kutokana na kipigo cha mwenza wake; mume ana rafiki yake wa kiume na pengine hata ndugu yake wa karibu kutoka katika familia moja.

Idadi hii inatisha, lakini ndiyo takwimu zinazotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Masuala ya Wanawake (UN- Women). Hizi ni takwimu za mwaka huu ambazo zimesambazwa na shirika hilo.

Pamoja na kuwepo kwa takwimu hizo, UN-Women linaeleza kuwa mwanamke mmoja kati ya wanne duniani wamekuwa wakikumbwa na vipigo, kuteswa, kunyanyaswa na kuuawa na wenzi. Kwamba kati ya hao, ni asilimia zisizozidi 10 ndiyo huamua kwenda kuripoti kwenye ngazi za mamlaka – ikiwamo Polisi, matukio hayo mabaya.

UN-Women inaeleza kuwa kwa mwaka jana pekee, inakadiriwa kuwa karibu wanawake na wasichana 45,000 duniani waliuawa na wapenzi wa karibu au wanafamilia.

Ingawa idadi hii ni ya kushangaza, ripoti iliyotolewa kwa pamoja na Ofisi ya Umoja wa Mataifa kuhusu Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) na UN-Women inafichua kwamba kiwango cha kweli cha mauaji ya wanawake kinaweza kuwa kikubwa zaidi.

Afrika ni eneo la pili baada ya Asia, kurekodi visa vya mauaji ya wenzi wa karibu wa kike.

Hata hivyo, Afrika inachukuliwa kuwa eneo lenye kiwango cha juu cha unyanyasaji, kwa kuwa mambo mengi ya kikatili hufanywa kwa siri kubwa na wahusika wa kuumizwa hutishwa ili wasisema hadharani.

“Wanawake na wasichana wa Afrika wako katika hatari kubwa ya kuuawa na wapenzi wao wa karibu au wanafamilia wengine kutokana na mazingira kadhaa, ikiwamo ukimya wa wale wanaofanyiwa ukatili,” inaeleza ripoti hiyo.



Ummu Mwalimu, Waziri wa Afya

Upungufu wa takwimu umeonekana kuwa changamoto, kwani kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, kati ya mauaji ya wanawake 81,000 yanayokadiriwa mwaka 2021, wanne kati ya kumi, hawana ‘taarifa za muktadha’ kuruhusu kutambuliwa na kuchukuliwa kuwa mauaji yanayohusiana na jinsi.

“Takwimu kuhusu mauaji yanayohusiana na jinsi yanayofanywa katika jamii, hasa wanaume kua wake ama wenza wao ni chache sana, hivyo kufanya kuwa vigumu kutambua idadi kamili ya wanaonewa na kupoteza maisha kutokana na matukio ya kikatili,” inaongeza ripoti hiyo.

Umoja wa Mataifa umekuwa ukitoa mwito kwa jamii kuacha ukatili wa kijinsi kwani huleta mparaganyiko mkubwa katika ujenzi wa familia.

UN-Women, imekuwa ikishirikiana na serikali kuhakikisha kuwa wanaoonea wanawake wanafikishwa katika ngazi za hukumu – hasa mahakama ili kupata adhabu kulingana na makosa ya kikatili yanayofanywa kwa wanawake.

“Natoa mwito kwa serikali na washirika wa Umoja wa Mataifa kote duniani kuongeza ufadhili wa muda mrefu na msaada mkubwa kwa mashirika yanayotetea haki na ustawi wa wanawake na watoto,” anaeleza Mkurugenzi Mtendaji wa UN-Women, Sima Bahous.

Sensa yasahau mahunta

Na Deusedith KAHANGWA

SENSA ya idadi ya watu wa Tanzania iliyofanyika Agosti 23, mwaka huu – kama ilivyokuwa kwa miaka yote, haikuhusisha kutambua idadi ya watu wenye jinsi mbili, maarufu “mahunta.”

Mahunta hujumuisha watu wenye jinsi mbili; ya kike na kiume kwa wakati mmoja na hawa huwekwa kwenye kundi la walemavu. Pengine huitwa majike-dume au madume-jike.

Pamoja na kwamba serikali imekuwa ikionekana kuwaweka kando, lakini ukweli ni kwamba watu hao wapo na idadi yao huenda inaongezeka kwa kasi. Sayansi inawatambua kwamba kuwa na hali hiyo ni ulemavu wa kawaida.

Kawaida, Tanzania hufanya sensa ya watu wake kila baada ya miaka 10.

Kwa mujibu wa Mapatano ya Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watu wenye ulemavu ya mwaka 2006, watu wenye ulemavu ni watu ambao wana dosari ya muda mrefu katika viungio vya mwili, akili au milango ya fahamu, inayowafanya washindwe kushiriki katika maisha ya jamii kama watu baki wanavyofanya. Tanzania imeridhia mapatano haya.

Kwa sababu hii, madodoso ya sensa na makazi ya watu yanayotumika Tanzania tangu miaka ya nyuma hukusanya taarifa za aina saba za ulemavu. Aina hizo ni ualibino, kuona, kusikia, kutembea, kukumbuka, kujihudumia, na kuwasiliana.

Aidha, madodoso haya hutoa nafasi ya serikali kupokea taarifa za “aina nyingine ya ulemavu,” japo madodoso hayo hayafanui aina hizo zinginezo za ulemavu.

Kwa kutumia utaratibu huu, takwimu zinaonyesha kwamba, mwaka 2002 Tanzania ilikuwa na walemavu 676,502; wakati mwaka 2012 walemavu waliuwa 3,157,516.

Hata hivyo, takwimu zote za nyuma, pamoja na takwimu za awali zilizotolewa



na serikali Oktoba mwaka huu, hazionyesha idadi ya walemavu katika kundi la mahunta, yaani majike-dume na madume-jike.

Kwa sababu hii, wataalam wa masuala ya idadi ya watu, wamekosoa utaratibu wa kukusanya takwimu za sensa ya watu na makazi kwa hoja kwamba jinsi ya kike na jinsi ya kiume siyo jinsia pekee za watu wanaozaliwa na kuishi nchini Tanzania.

Gazeti la Mwananchi toleo la Machi 28, 2017 liliripoti juu ya “Mtanzania mwenye utata wa jinsi” – ambapo habari hii ilionekana yenye utata, lakini ukweli ni kwamba ilikuwa sahihi kwa kuwa mhusika alizaliwa akiwa na jinsi mbili.

Gazeti la HabariLeo, toleo la Desemba 2017, liliwahi kuripoti juu ya mtoto mwenye jinsi mbili alifanyia upasuaji kwa ajili ya kurekebisha jenitalia zake, katika Hospitali ya Muhimbili, Dar es Salaam.

Pia mwaka 2010, huko Shinyanga, kulitokea mfungwa aliyehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela, huku akiwa na jenitalia za kike na kiume.

Gereza aliloamuriwa kufungwa halikuwa na utaratibu wa kuwahudumia wafungwa wa aina hiyo, na matatizo kama haya hujitokeza shuleni, na

Sensa yasahau mahunta

hospitalini pia, maana huko hakuna wodi za mahunta.

Mshauri nasaha na mtetezi wa haki za binadamu, Dkt. Julius Kamhamba wa Dar es Salaam anaeleza kuwa mtu kuzaliwa akiwa hunta, hakuna maana kwamba ni shoga ama msagazi, bali ni ulemavu.

“Anaeleza kuwa mahunta hawana uhusiano wowote na mashoga wala wasagaji, kwani wao wanazaliwa wakiwa hivyo na hawarithi wala kufunzwa wakiwa watoto ama ukubwani, ni hali ya kuzaliwa,” anaongeza.

Profesa Elof Axel Carlson kutoka Chuo Kikuu cha New York, Marekani anasema kuwa; “jinsi ya mtoto kwenye cheti cha kuzaliwa, haiendani na ukweli wote kuhusu ujinsi wa kibayolojia, kwani cheti cha kuzaliwa kinatambua jenitalia za nje, tena zile zinazotambuliwa kisheria pekee.”

Anasema kuwa karibu “asilimia moja ya watoto hazaliwa wakiwa na utata wa kijinsi katika ngazi ya kromozomu na kwenye jenitalia zao.”

Profesa Carlson anawataja watoto hawa, kama “mahunta’ wa aina tatu; kwanza, kuna mahunta wenye jenitalia ya kike na kiume na zote zikiwa hai; pili, kuna mahunta wenye jenitalia ya kike na kiume, wakati jenitalia ya kike pekee ikiwa hai; na tatu, mahunta wenye jenitalia ya kike na kiume, wakati jenitalia ya kiume pekee ikiwa hai.

Kwa mujibu wa Prof. Carlson, endapo hesabu zitatumika Tanzania yenye watu 61,741,120, huenda kuna watu wapatao 617,411 wenye ujinsi tata, na ambao takwimu za sensa na makazi zinawasahau kila mwaka.

Muhtasari wa takwimu za sensa tangu 1967

Sensa ya watu na makazi ni utaratibu wa kukusanya, kuchakata, kuchambua, kutathmini, kuchapisha, kusambaza na kutunza takwimu za kidemografia, kiuchumi na mazingira wanayoishi watu katika nchi kwa kipindi maalum.

Utaratibu huu huiwezesha serikali

kupata mchanganuo wa taarifa za msingi kama vile idadi ya watu na namna ya kusambaza huduma za kijamii kwa kuzingatia umri, jinsi, hali ya ulemavu, hali ya elimu, shughuli za kiuchumi, hali ya makazi, vizazi, vifo na vigezo vingine zinavyoainishwa katika dodoso la sensa.

Hatimaye, serikali hutumia takwimu hizi kuandaa mipango ya maendeleo yenye viashiria vya ufanisi sahihi kwa kila sekta na makundi mbalimbali ya kijamii kama vile watoto, vijana, wanawake, wazee na walemavu.

Kumbukumbu zinaonyesha kwamba, katika kipindicha miaka 61 ya kuzaliwa kwa Tanzania, tayari sensa ya watu na makazi imefanyika mara sita, kila baada ya miaka 10, yaani mwaka 1967, 1978, 1988, 2002, 2012 na 2022.

Kitaifa, mwaka 1967 kulikuwa na watu 12,313,469; mwaka 1978 kulikuwa na watu, 17,512,610; mwaka 1988 watu 23,095,878; mwaka 2002 watu 34,569,232; mwaka 2012, watu 44,928,923; na mwaka 2022, watu 61,741,120.

Kuhusu uwiano wa kijinsi, mwaka 1967 kulikuwa na asilimia 51.11 ya wanawake; mwaka 1978 kulikuwa na asilimia 50.38 ya wanawake; mwaka 1988 kulikuwa na asilimia 50.24 ya wanawake; mwaka 2002 kulikuwa na asilimia 51.14 ya wanawake; mwaka 2012 kulikuwa na asilimia 51.32 ya wanawake; na mwaka 2012 kulikuwa na asilimia 51.32 ya wanawake.

Na kwa mujibu wa taarifa ya awali ya sensa na makazi ya watu iliyotolewa na serikali mwezi Oktoba mwaka huu, mchanganuo wa idadi ya watu, kwa kuzingatia huduma za jamii, anaonyesha mgawanyo wa takwimu ufuatao:

Zahanati 7,965; vituo vya afya 1,466; hospitali 676; shule za msingi 19,769; shule za sekondari 5,857; majengo ya ghorofa 68,724; majengoyasiyo ya ghorofa 13,540,363; majengoyanayoendelea na ujenzi 739,285; majengo yenye anwani za makazi 10,751,123; na majengo yasiyo na anwani za makazi 3,597,249.

Nguzo za demokrasia na uchaguzi

Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA

LEO nazungumzia nguzo za tano ambayo ni chaguzi za vipindi. Chaguzi za jinsi hii ni muhimu kwa sababu kuu mbili; kwanza, ili kuheshimu na kutunza matakwa na maoni ya umma. Pili, ili kuthibitisha na kuhisha uhalali wa serikali na watawala kwa watu.

Taratibu za chaguzi ikiwemo vipindi vyake, lazima vionyeshwe wazi katika katiba. Ni muhimu kuzingatia kanuni mojawapo ya chaguzi, kwamba kila raia anayo haki sawa ya kuchagua serikali kwa kupiga kura na kwamba kila mwananchi ana haki ya kugombea na kuchaguliwa kushika nafasi ya uongozi.

Uchaguzi ni mchakato mrefu unaosimamiwa na mamlaka na vyombo mbalimbali, ikiwamo tume ya uchaguzi, msajili wa vyama vya siasa, Polisi na vyombo vingine vya usalama, watawala walioko madarakani na kiwango cha mamlaka zao na mengineyo.

Pasipo uwepo wa katiba nzuri, hizo chaguzi za vipindi ni kama maigizo tu na wala siyo sura ya demokrasia.

Kuna vigezo kadhaa ambavyo vinakuwemo katika katiba kama sifa za mpiga kura na mgombea. Vigezo hivyo na sifa ndivyo huwaruhusu ama wengine kupiga kura na kugombea nafasi za uongozi au kuwanyima nafasi hizo.

Wajibu mkubwa wa serikali ni kuhakikisha kwamba inajengea raia wake sifa za kushiriki chaguzi. Msingi wa demokrasia ni ushiriki wa watu, hivyo ni muhimu ziwepo kanuni zinazotoa fursa ikiwezekana kwa raia wote kuwa na sifa.

Kwa mfano, kiwango cha elimu ni moja ya vigezo, basi ni muhimu kuweka kiwango cha elimu ambacho wengi (au wote) watakuwa nacho.

Utawala wa demokrasia malengo yake ni kujenga utawala makini na fanisi ambao ni shirikishi, wa wazi, na unaozingatia sheria ili kuleta maendeleo ya pamoja.



Kwa hiyo, demokrasia imara hutegemea watu wenye maarifa na wanaotambua haki zao. Demokrasia ya wajinga ni hatari kwa ustawi wa taifa. Ndio sababu nimesema kwamba wajibu mkubwa wa serikali ni kuwajengea raia wake wengi (au wote) maarifa kwa kuwapatia elimu nzuri. Inapofikia hatua ya kukubaliana kwamba mgombea wa ubunge awe anajua kusoma na kuandika tu, ni kukiri kuwa taifa liko chini kielimu. Kadiri taifa linavyoongeza viwango vya elimu ya raia wake (elimu bora) ndivyo inavyojitengenezea kitako kipana zaidi cha kujipatia wapiga kura bora na viongozi bora.

Katika kuwezesha chaguzi za vipindi kutimiza malengo ya mfumo wa utawala wa kidemokrasia ni muhimu sana katiba zive nzuri kwa maana ya kulinda tunu za msingi za demokrasia.

Hii ina maana kuwa ni muhimu sana katiba iweke miundo na mamlaka za chaguzi ambavyo vinafikisha taifa kwenye matokeo yaliyokusudiwa ya uwepo wa mifumo ya demokrasia.



Ujasiri wa Bashiru unabeba mengi

MOJA ya mada zinazotawala anga za habari nchini Tanzania ni kauli ya hivi karibuni ya Katibu Mkuu wa zamani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Bashiru Ally, aliyenukuliwa akieleza kukerwa na watu wanaosifia viongozi wa sasa wa nchi, ikidaiwa kumlenga kumlenga Rais Samia Suluhu Hassan.

Awali nilidhani labda kada huyo alinukuliwa vibaya, na nikatarajia kumsikia akikanusha habari hiyo.

Hata hivyo, hadi wakati ninaandika makala haya, Dkt. Bashiru hajakanusha habari hiyo.

Namfahamu Dkt. Bashiru kabla hajaingia kwenye siasa. Nilikutana naye mara ya kwanza mwaka 2005.

Katika muda mfupi wa maongezi naye, ilikuwa bayana kwangu kwamba msomi huyo ni hazina kubwa kwa taifa letu, na sikuwa na shaka kwamba huko mbeleni atakuwa profesa.

Ni katika mazingira hayo, alipoteuliwa kuwa katibu mkuu wa CCM, Mei 2018, nilifadhaika kwa sababu kada ya taaluma ya elimu ilimpoteza msomi muhimu.

Kuhusu yeye kuonekana kukerwa na wanaomsifu Rais Samia - "(Mama) kuupiga mwingi", binafsi ninaona mambo makuu manne.

Kwanza, Dkt. Bashiru ametumia haki yake kikatiba kutoa maoni yake.

Pili, haki huambatana na wajibu. Na kama Mtanzania, hakuna wajibu aliokiuka, hali ni tofauti ndani ya CCM. Ni wazi mwanasiasa huyo anafahamu kuwa ni "kosa la uhaini" kumkosoa hadharani mwenyekiti wa taifa wa chama hicho ambaye pia ni Rais wa Tanzania.

Tatu, alichofanya Dkt. Bashiru

kinaweza kutafsiriwa kuwa ni unafiki, kwa sababu hakuwahi kuwakemea waliomsifu "bosi wake wa awali" Rais John Magufuli (sasa marehemu).

Kimsingi, baadhi ya waliomsifu Magufuli walikwenda mbali hadi kukufuru, ambapo waziri mmoja wa zamani alimuita mkuu huyo wa nchi "mungu", RC mmoja akasema "Mungu ndiye anapaswa kumshukuru Magufuli" na kiongozi mmoja wa dini ya Kiislamu akasema "Magufuli ni zaidi ya Yesu Kristo na Mtume Muhammad." Ushahidi wa kauli hizo upo mtandaoni.

Nne, kauli ya Dkt. Bashiru ina mantiki, kwamba hii kasumba iliyozuka ya kusifu viongozi "kupitiliza" inakera. Kama hatuwasifu madaktari kwa kutibu, walimu kwa kufundisha, na wanataaluma wengine, iweje tumsifu kiongozi kwa kutimiza kazi "tuliomwajiri" afanye?

Mfano, kiongozi wa umma anapoidhinisha matumizi ya fedha za walipakodi, siyo kwamba anazitoa kwenye mshahara wake; sasa hizo shukrani zinatoka wapi kama siyo unafiki! Zinakera.

Lakini hili halijaanzia kwenye utawala wa Rais Samia. Limekuwepo miaka nenda miaka rudi, japo lilstawi zaidi zama za Rais Magufuli.

Wakati ni sasa wa kuacha kusifu pasipostahili, hasa kama kiongozi anatimiza wajibu wake wa kikatiba. Tubadilike.

Hata hivyo, swali kubwa linabaki - "Je, Dkt. Bashiru amepata wapi ujasiri huo ilhali anafahamu fika athari za alichokifanya?" Muda utaeleza (time will tell).

Walioibiwa laptop watakiwa Polisi

Na Waandishi WETU

JESHI la Polisi limewataka abiria waliopoteza mizigo yao kwenye ajali ya ndege ya Precision Air mjini Bukoba kuripoti kwa ajili ya uchunguza zaidi.

Gazeti la Pambazuko Jumatatu iliyopita lilikuwa la kwanza kuandika habari kubwa iliyoeleza kuwepo kwa wizi wa mizigo ya baadhi ya abiria waliopatwa na ajali hiyo.

Wengi wa manusura wa ajali hiyo iliyosababisha vifo vya watu 19, waliliambia Pambazuko kuwa walipoteza mabegi na kati yao, 13 walipoteza kompyuta mpakato (laptop).

Ajali ya ndege hiyo ilitokea Novemba 6, mwaka huu – nje kidogo ya Uwanja wa Ndege wa Bukoba, baada kutua kwa dharura ndani ya Ziwa Victoria kutokana kile kinachoelezwa na wataalamu kuwa ni kuwepo kwa hali mbaya ya hewa.

Pambazuko lilimtafuta Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kagera, William Mwampaghale kutaka kufahamu jeshi hilo linafanya nini hadi sasa kuhusu hatma ya kupatikana kwa mizigo iliyoibiwa; nani waliiba; kwanini na zaidi sana wahusika kama wamekamatwa?

Kamanda William kwanza alishangaa kupigiwa simu kuhusu wizi wa mizigo iliyotokea kwenye ajali ya ndege, akieleza kwamba jeshi lake linahusika zaidi na ajali za barabarani.

Pambazuko lilijikita katika tukio la wizi na siyo ajali, lakini Kamanda William alisema siyo sahihi kuulizwa Polisi.

“Kuhusu hili, unempigia msemaji wa serikali, ndugu Msigwa (Gerson), yeye ndiyo msemaji kuhusu kila kitu kwenye ajali hii, kunipigia mimi siyo sahihi, kama ingekuwa ni ajali ya barabarani sawa, sasa hii ni ndege,” alisema kamanda William.

Hata hivyo, baadaye kidogo akaongeza; “sisi hatuna taarifa za wizi

huo, huenda wapo waliozisoma kwenu Pambazuko, lakini tunasubiri taarifa za hao wanaolalamika kuibiwa laptop na mizigo yao mingine ili tuanze uchunguzi wetu.”

Alitoa mwito kwa wote walioibiwa mizigo kufika kwenye vituo vya Polisi ambako wataandika maelezo yao na kazi ya kuchunguza itaanza mara moja.

“Tukipokea taarifa, tutaanza kazi mara moja na haraka zaidi lakini kama hakuna anayelalamika, tunafanyaje kazi sasa kwa mazingira ambayo hatujui wizi ulitokeaje na labda lini ulifanyika,” ameongeza kiongozi huyo wa Polisi wa mkoa.

Pambazuko lilimtafuta (kwa njia ya simu) Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa Jumamosi – saa 6.26 mchana ambapo simu yake ya mkononi iliita tu bila kupokelewa. Baadaye tena – saa 8.18, gazeti hili lilipigia simu yake ya mkononi ambapo ilisikika kuita bila kupokelewa.

Namna mizigo ilivyotolewa

Pambazuko linazo taarifa za uhakika kuwa baadhi ya mizigo ya abiria; walionusurika na wale waliopoteza maisha, ilikusanywa kutoka kwenye ndege hiyo iliipelekwa hospitali hapo ni pamoja na mabegi yaliyokuwamo kwenye eneo la abiria (cabin) na mingine iliyokuwa eneo mahsusi kutunza mizigo (luggage compartment).

Pambazuko liliwatafuta baadhi ya walionusurika kwenye ajali hiyo na kuwahoji kuhusu usalama wa mizigo yao, na wengi walikiri kupokea, lakini mingi ikiwa imefunguliwa na kutolewa baadhi ya vitu, hasa vyenye thamani, zikiwamo laptop.

Daktari Felix Otieno alikiri kupata mizigo yake, lakini begi lililokuwamo ndani ya eneo la kuketi abiria, halikuwa na laptop, na kwamba aliletewa akiwa hospitali.

Walioibiwa laptop watakiwa Polisi



Ajali

“Mimi niliambiwa mizigo yetu imekusanywa mahali hapo hospitali tulipokuwamo, lakini nilipokagua yangu, sikukuta laptop, na sikuwa na muda wa kuuliza maana bado nilikuwa na kiwewe, na hata sasa sijui nani aliichukua,” aliliambia Pambazuko.

Ofisa mmoja wa Mradi wa Bomba la Mafuta la Tanzania na Uganda (Eacop) ameliambia Pambazuko kuwa mfanyakazi wao mmoja, raia wa Uingereza ambaye alikuwa mmoja wa marehemu, Jonathan Rose, kwenye mizigo yake kulikosekana laptop.

“Jon alikuwa na laptop, na kwa kazi zake, ni lazima kuwa na kifaa hicho kwa ajili ya kazi, lakini begi lake halikuwa na laptop, na hata wakati linachukuliwa pale hospitali, lilionekana kufunguliwa,” anaongeza huku akikataa kutajwa jina gazetini.

Ndugu wa Aneth Kaaya, binti aliyekuwa akielekea Bukoba kujitambulisha ukweni, inaelezwa na ndugu zake kwamba hakuwahi kusafiri bila laptop, lakini

wakati wanakabidhiwa mizigo ya ndugu yao, hawakuona laptop yake.

Mwingine ambaye laptop yake haikuonekana ni manusura Eva Mcharo, mtumishi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru). Huyu anaeleza kuwa mizigo yake ilikutwa imefunguliwa na hakukuwa na laptop.

Wengine ni watumishi watano wa Menejimenti na Maendeleo ya Afya (MDH), waliokuwa wakifanya kazi makao makuu, Dar es Salaam; hawa inaelezwa kuwa wote walikuwa na laptop, lakini kwenye mizigo iliyokusanywa na kukabidhiwa, hakukuwamo vifaa hivyo muhimu kwa ajili ya kazi.

Wafanyakazi wote hawa walifariki dunia ambao ni pamoja na watafiti watatu wakiwemo Dkt. Boniface Jullu, Dkt. Neema Faraja na Dkt. Alice Simwinda pamoja na Sauli Happymark pamoja na mkuu wa kitengo cha mawasiliano, Zarcharia Mlacha.

Watumishi wa MDH ambao ni

Walioibiwa laptop watakiwa Polisi

manusura na kwamba nao walipoteza laptop zao ni Nickson Jackson, Dkt. Josephine Mwakisambwe na Dkt. Felix Otieno.

Manusura mwingine, Emil Mwesiga anashangaa iweje watu wahangaika na laptop ambazo huenda hata zisifanye kazi kwani nyingi zitakuwa zililowa maji.

“Nashangaa binadamu sijui tumekuwaje, watu wanahangaika kuiba mali za watu waliopata ajali, na sijui zinawasaidia nini, ni ajabu sana,” anaongeza huku akionekana kukwerwa na tabia hiyo.

Pambazuko ambalo liliwahi kufika eneo la tukio muda mfupi baada ya ndege hiyo kutua majini, halikuona


waokozi wakihangaika na mizigo na hata manusura hawakutoka na mizigo, hivyo mingi ilibaki ndani ya ndege hadi gazeti hili linaondoka eneo la tukio.

Juhudi za kupata uthibitisho wa nani alimuru mizigo hiyo itolewe bila kuwepo usalama wa uhakika na ipelekwe hospitali badala ya kuhifadhiwa mahali pengine, ziligonga mwamba baada ya uongozi wa uwanja wa ndege wa Bukoba kusema upewe muda kufuatilia.

Kumekuwepo mazoea ya baadhi ya wananchi kugeuza ajali za magari, hasa ya abiria kuwa “chumio” kwa kuiba mali za manusura na hata wanaofariki dunia, tabia ambayo imekuwa ikikemewa kwa nguvu na jamii.



Watoto walindwe kwa nguvu zote



Na Jabir IDRISSE

HEBU fikiria unapata picha gani tukio kama hili; mkazi wa Mtaa wa Magomeni, Hahabu Matesi mwenye umri wa miaka 33 amehukumiwa kifungo cha miaka 20 jela kwa kosa la kumuingilia kinyume cha maumbile mtoto wa kike wa umri wa miaka 6?

Huyu mtoto hajielewi kwa lolote. Hana kosa na mtu yeyote. Kule kuwa umri wake ni mdogo anakosa kujitetea, ndiko kumemponza na kujikuta akiishia mikononi mwa mtu mzima aliye na akili zake na wakati mwingine mwenye familia yake ya mke na akiwa na watoto.

Huu ni ujinga mkubwa na ishara ya watu kuchoka kufikiri na sasa kuamua kurithi hulka za kishenzi na kijahili, na kuwageukia watoto kwa kuwahujumu.

Katika upande mwingine unasikia eti Jecha Umari Maliwana mwenye umri wa miaka 65 anayeishi Kinyasini Mkoa wa Kaskazini Unguja, Zanzibar, amefikishwa mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mkoa ya Vuga, Hakimu Jaribu Mpakani, na kusomewa mashtaka mawili; kumtorosha

msichana wa umri wa miaka 13 na kosa la pili la kumuweka kinyumba msichana huyo na kila siku, kwa wiki nzima - akimbaka.

Umeona vizuri hiyo picha? Ni hivi - babu mzima aliyekula chumvi nyingi, ameshikwa na dola akituhumiwa kwa makosa hayo mawili. Unaona zinaingia akilini wewe hizi taarifa mbili? Kwamba siku hizi shetani kapiga kambi ndani ya akili za watu wazima na kuwaamulia kuwa watu katili dhidi ya watoto wakiwemo wale waliowazaa?

Ajabu utasikia eti yule jamaa kashikwa na shetani kwamba amekuwa hamnazo na anatomikia utamaduni wa "kuku kula vifaranga vyake?"

Hakika binadamu wamebadilika hata kumshinda huyo shetani ambaye desturi yake ni kumbamba mtu yule ambaye tayari kwa hiyari yake amefikiria na kupanga kutenda uovu kwa sababu anazozijua.

Matukio mengine ni kama ya kuwakung'uta makonde na kuwanyima chakula kwa kisingizio hiki au kile.

Watoto walindwe kwa nguvu zote**Inatoka Uk. 13**

Au baba kumfungia ndani mtoto wake kwa sababu ameiba pesa ya chumvi na kiungo. Ni matukio mabaya yanayohitaji kukomeshwa.

Kwa sababu ya matendo haya mabaya - matukio yanayoimiza watoto yanazidi kuongezeka ndio maana kukawa na mipango jumuiishi ya kuyakomesha.

Sasa kunatekelezwa kampeni ya kukomesha ukatili dhidi ya wanawake na watoto; wote wa kike na wa kiume. Watoto wanahitaji kinga na kuhamiwa ili wakue vizuri na kupata haki yao muhimu ya elimu, kati ya haki zao za msingi kama binadamu.

Kampeni inakusudiwa kumaliza utamaduni na hulka za kishenzi za kuwahujumu watoto ambao kweli inaaminika ni hazina muhimu kwa mataifa yao leo na kesho.

Taifa linakuaje likiacha watoto kuendelea kuimizwa na kukosa kabisa fidia ya maumivu wanayoachwa nayo baada ya mikono ya watu wazima kuwashukia?

Ni uamuzi wa dhati wa Umoja wa Mataifa (UN) kwamba mataifa yazitumie ‘Siku 16’ za kila mwaka (kuanzia Novemba 25 hadi Desemba 10), kutafakari namna bora ya kushikamana na kupanga mikakati ya kukomesha ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Siku hizi zimekuwa zikitumika kutangaza mabaya ya kukandamiza kwa kumizwa kingono, kimwili na hata kauli dhidi ya ustawi wa wanawake na watoto na katika siku hizo, taasisi nyingi, ikiwamo serikali hutumia kuhimiza usawa, kutobagua jinsi, kuonea na kukomeshwa kwa kila aina ya ukatili dhidi ya makundi hayo.

Ni rai ya PAMBAZUKO kwamba pamoja na mipango hiyo panahitajika mkazo sana wa wale watendaji wa mamlaka za utoaji wa haki pale mtuhumiwa wa matendo haya mabaya dhidi ya watoto, anaposhikwa na kupelekwa mahakamani.

Imekuwa tatizo kubwa watuhumiwa

kuachiwa huru kwa kesi zao kutohibitishwa baada ya kiitwacho “ushahidi ulikuwa dhaifu” au utasikia hakimu akisema “upande wa mashitaka haukuwasilisha ushahidi madhubuti wa kuishawishi mahakama kuwatia hatiani watuhumiwa.”

Hii inaeleweka pasina shaka kwamba mahakama haina haki ya kumtia hatiani mtuhumiwa ambaye hajaguswa na ushahidi; bali hatia hujengwa na ushahidi uso shaka unaowasilishwa na mwendesha mashitaka.

Mshikamano wa asasi hizi za kidola - Jeshi la Polisi, Serikali, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahakama ni jambo la muhimu sana katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Watendaji wa taasisi hizo za kidola wakiungana na kuwajibika ipasavyo kuna uwezekano mkubwa wa ushindi dhidi ya ukatili kwa wanwake na watoto ukapatikana.

Lakini lipo tatizo linalokua siku hizi; mtindo wa wazazi au walezi kujiachia na kuamua kutibu njaa zao kwa kuangusha mabega yao kwa watanda maovu hao na kukaa na kujadiliana suluhu – mara nyingi wakipewa pesa ili kufunika matendo maovu. Hili likomeshwe pia.

Hivi wazazi na walezi mnapoamua hivyo mmeiweka wapi hadhi ya mtoto aliye dhalilishwa? Mmemfikiria huyu mtoto lini atasahau maumivu aliyosababishwa na waovu? Hapana na hapana kabisa.

Ijulikane wazi kwamba mtoto anayeumizwa kwa vitendo vya kumdhalilisha hata akipona majeraha, basi hubakia na fikra za tukio alolotendewa kwa maisha yake yote. Hawezi kusahau na inapokuwa ametendewa uovu na mtu anayemfahamu, inakuwa shida zaidi.

Mtu aliyemtendea ubaya mtoto; iwe wake mwenyewe au siyo wake, abanwe kisawasawa maana hastahili heshima wala hadhi ambayo ameua vyote hivyo na kubakia mkatili na mshenzi.

Pambazuko

Gazeti la Pambazuko sasa kupokea matangazo

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi kwa

kuwasiliana kupitia namba hii:
0744 768 263 au Barua- Pepe;
info@pambazuko.tz

*Karibu sana Pambazuko isaidie
kupaisha na kupambazua
huduma na biashara yako.*

Watoto hubeba akili za mama

INAWEZA kushangaza, lakini ndiyo lukweli wa kisayansi kwamba akili za watoto, sehemu kubwa hutoka kwa mama zao kuliko baba.

Utafiti wa kisayansi unaonyesha kwamba kwa sehemu kubwa, akili ya watoto hutoka kwa wazazi wa kike kupitia kromozomu yao ya "X," badala ya kutoka kwa wazazi wa kiume kupitia kromozomu yao ya "Y."

Wataalamu wa bayolojia wanaeleza kuwa urithi wa kibayolojia ni uhamisho wa sifa za kitabia na kimaumbile kutoka kwa wazazi kwenda kwa watoto.

Sifa hizo nia pamoja na urefu, unene, rangi ya ngozi, rangi ya nywele, kipara, aina ya damu, magonjwa kama vile selimundu na jinsi.

Uhamisho wa sifa hizi kutoka kwa wazazi kwenda kwa mtoto hufanyika kupitia seli za uzazi, yaani mbegu za kiume (spematozoa) na mayai ya kike (ovamu).


Wanasayansi wanasema kwamba, spematozoa inazo kromozimu 23, na kwamba ovamu inazo kromozimu 23 pia.

Wanafafanua kuwa, baada ya urutubusho, huzaliwa 'kijusi' chenye kromozomu 46, ambapo kromozomu 44 ni seli zinazoratibu michakato ya kimwili na kromozomu mbili zinazoratibu michakato ya kijinsi katika mfumo wa uzazi.

Kwa mujibu wa wataalamu hawa, kama mtoto ni wa kiume, kila seli ya mwili wake inayo jozi moja ya kromozomu yenye fomati ya "XY" yenye kuashiria jinsi yake ya kiume. Na kama mtoto ni wa kike, kila seli yake ya mwili inayo jozi moja ya kromozomu yenye fomati ya "XX" yenye kuashiria jinsi yake ya kike.

Hivyo, utaona kuwa, kama ovamu itachangia maudhui ya kijenetiki yenye fomati ya "X" mara mbili, spematozoa itakuwa imechangia maudhui ya kijenetiki yenye fomati ya "X" mara moja.

Na sasa, kwa kuwa utafiti wa kisayansi unaonyesha kuwa akili ya watoto hutoka kwa wazazi kwenda kwa watoto kupitia



Mbegu za uzazi

kromozomu ya "X," inafuata kimantiki kwamba, mama anayo nafasi kubwa ya kuambukiza watoto wake akili zake kuliko nafasi aliyonayo baba.

Utafiti mmoja uliofanywa na Baraza la Utafiti wa Kitabibu, kwenye Chuo Kikuu cha Glasgow, Uingereza umeonyesha kwamba akili za watoto, mara nyingi hufanana na akili za mama zao.

Matokeo ya utafiti huo yalionyesha kwamba, kwa sehemu kubwa, kisababishi kikubwa cha akili za watoto ni mama.

Hata hivyo, utafiti huu umekosolewa na baadhi ya wadadisi wa sayansi ya uzazi kwa sababu kwamba, kuna vigezo zaidi ya vinasaba katika kuamua akili ya mtoto.

Kwa mfano, kulingana na tovuti ya Psychology Spot (<https://psychology-spots.com>), ni kati ya asilimai 40 na asilimia 60 pekee ya akili ya mtoto hurithiwa kwa njia ya vinasaba.

Kwa hiyo, wakosoaji hawa wanawafariji wazazi wa kiume na kuwahimiza kutumia muda mwingi kuwaambukizi watoto akili zao kupitia fursa hiyo ya asilimia 40 zilizobaki.

***Makala hii imepatikana kutoka vyanzo mbalimbali vya mtandao.**

Amua kifo chako. Nenda Kaole

Na Scovya MANASE

IMANI zimekuwepo tangu mwanzo wa dunia. Hakuna anayeweza kueleza kwamba ameleta imani bora zaidi mahali popote, kwani waliokuwepo walikuwa na namna ya kuamini na mambo yakatokea.

Wazungu pamoja na kudai kuwa wao walileta “imani ya kweli Afrika,” lakini uhakika ni kwamba walikuta bara hilo likiwa na imani zake na namna watu wale walivyokuwa wakiabudu kwa namna ambayo waliamini.

Mji wa Bagamoyo, ulioko Mkoa wa Pwani, Tanzania ni miongoni mwa maeneo ya mwanzo kabisa kufikiwa na Waarabu na Wazungu kutoka Bara Asia na Ulaya, waliofika baada ya karne ya 12.

Waarabu kama ilivyokuwa kwa Wazungu, walikuja na njia zao za kuabudu; wakileta dini ya Uislam na Ukristo, mtawalia. Wapo watu waliowaamini, lakini pia wapo waliogoma kukubali imani zao, kwani nao walikuwa na zao.

Upo ushahidi kwamba wakazi wa Bagamoyo, kama ilivyokuwa maeneo mengi ya Tanzania, walikuwa na dini na imani zao. Waliomba masuala kadhaa kwa Mungu na baadhi walifanikiwa kwa imani na wengine hawakuambulia lolote kwa imani ileile; hawa kundi la pili wakielezwa kutotimiza baadhi ya masharti (amri).

Ndani ya Wilaya ya Bagamoyo, kipo kijiji kinaitwa Kaole ambacho kimesheheni historia ya imani anuai; kuanzia imani za kale, imani mpya; Uislam na Ukristo zilizoletwa na wageni.

Moja ya historia ya kuvutia ndani ya makumbusho ya historia Kaole, ni kuwepo kwa mbuyu ambao unaelezwa kuwa na zaidi ya umri wa miaka 500.

Historia inaelezwa kuwa mbuyu huo ndiyo ulikuwa nguzo ya imani kubwa kwa wakazi wa mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Morogoro na maeneo mengine, huku watu kutoka nchi jirani ikiwamo



Mbuyu

Kenya na Uganda wakiwasili Kaole kwa ajili ya tiba na “ushauri” mwingine.

Moja ya imani inayotajwa ni kwamba mbuyu huo ulikuwa ni chanzo cha mtu kuongeza umri au kuupunguza.

Kwamba ukifika katika mbuyu huo unatakiwa kunuia kile unachopenda kitokee kwako; ikiwa unataka maisha marefu zaidi, unatakiwa kuuzunguka mbuyu huo kuanzia kulia.

Kila mzunguko mmoja unapokamilika, unaongeza mwaka mmoja, hivyo unapouzunguka mara 10, unaongeza miaka 10 ya kuishi, kuanzia umri ulionao wakati wa zoezi la kuuzunguka.

Ikiwa unahitaji kupunguza umri wako, kwa sababu zozote zile, mhusika anatakiwa kuuzunguka mbuyu huo kuanzia kushoto. Kila mzunguko mmoja unapokamilika, basi unapunguza mwaka mmoja.

Zaidi ya kuongeza umri, mbuyu huo unatajwa kuwa mwanzo wa ishara za kufanikiwa ama kutofanikiwa - unachotakiwa kufanya ni kuchukua msumari na kuugonga kwa nguvu kwenye mti huo, endapo utazama, basi unafanikiwa mambo yako uliyonua. Ukipinda ama kukatika, “huna chako.” Ondoka!

Dawasco hebu oneni aibu kidogo

Mhariri,

WAKATI nikiendelea kuwa na hasira za kutumia kiasi kikubwa cha fedha kununua maji kwa miezi miwili kutokana na uzembe wa kufikiri wa Dawasco, nashangaa kupokea ankala ya maji kwa mwezi Novemba, 2022.

Ankala hii inanitaka kulipa Sh. 5,600 za maji kwa mwezi huo ambao sikupata hata tone la maji kutoka kwenye mtandao wa mabomba ya Dawasco. Mimi naishi Bunju, Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam.

Ninawashangaa Dawasco, iweje waniletee ankala ya maji kwa mwezi ambao sikupokea hata tone kidogo la maji kutoka kwao?

Hivi ni nini kinawasukuma Dawasco kutaka kuniibia pesa zangu? Pia naamini kabisa kwamba siko peke yangu kwenye kadhia hii.

Kwa mtazamo wangu, niliamini Dawasco wangukuwa wa kwanza kuomba samahani na kama kuna ankala yoyote kwa Novemba, basi wangesamehe – kutokana na usumbufu waliowapa wateja wao, lakini kumbe ndiyo wako 'bize' kuandaa ankala kwa maji hewa.

Enyi Dawasco, kuweni na aibu hata kidogo basi, acheni unyang'anyi wa pesa zetu tunazozipata kwa taabu sana.

**Michael Malamsha,
Bunju, Dar es Salaam.**

Hongera Pambazuko

Mhariri,

NIMEKUWA msomaji na mfuatiliaji mzuri wa gazeti lako la Pambazuko tangu kuanza kwake – mwanzoni mwa Julai, mwaka huu bila kukosa nakala yangu kila wiki.

Hakika Pambazuko limekuwa chanzo kikubwa cha maarifa na taarifa, siyo kwangu tu, bali kwa ndugu na jamaa ambao huwapa nakala.

Na uzuri zaidi, linapatikana bure, licha ya kuwa na hadhi ya kuuzwa kwa kiasi chochote.

Mussa Ibrahim.

Temeke, Dar es Salaam.

Treni ya umeme ni mthani

Mhariri,

NAENDELEA kuwa na wasiwasi kuhusu namna treni ya kisasa inayotumia umeme (SGR) itakavyofanya kazi katika mazingira ya kukatika-katika kwa nishati hiyo muhimu hapa nchini.

Zimekuwepo sifa kwamba treni hiyo ndiyo mwokozi wa majanga ya usafiri kwa abiria na hata mizigo - kwamba utakuwa wa uhakika, bei nafuu na zaidi sana kubeba mizigo mingi kwa wakati mmoja, huku ikiepisha uharibifu wa barabara zetu.

Sifa zote hizo ni sahihi, lakini shida moja kubwa; Tanzania yenye sifa nyingine ya kukosa ama kuwa na mgawo wa umeme kila mara, utaweza kuendesha treni hiyo?

Naamini wahusika, ambao ni serikali kupitia Shirika la Reli (TRC) limejipanga ili kuepusha taifa na aibu ya treni kushindwa kusafiri kutokana na kukosekana kwa umeme.

Vinginevyo niamini kuwa treni hizo zinakuja zikiwa na behewa moja lenye kubeba betri kubwa ama jenereta lenye uwezo wa kuiendesha hata unapatika umeme wetu.

**Juma Dihula,
Morogoro.**

Tunapokea Barua

Mhariri anapokea barua kutoka wasomaji wake kwa ajili ya kuzichapisha ama kuzitafutia majibu kutoka ofisi za serikali na binafsi. Tuma barua yako kwa njia ya barua-pepe: info@pambazuko.tx au kupitia namba ya simu: 0744 768 263

Zuma kurejea korokoroni?

JUMATATU iliyopita – Novemba 21, Mahakama ya Juu ya Rufaa nchini Afrika Kusini ilieleza kuwa uamuzi wa Kamishna wa Jeshi la Magereza kumwachia huru Jacob Zuma, rais wa zamani wa nchi hiyo, haukuwa sahihi.

Kamishna wa Magereza wa wakati huo, Arthur Fraser alimwachilia Zuma kutokana na sababu za kiafya na umri mkubwa.

Mahakama hiyo imeeleza kuwa msamaha huo ulikuwa kinyume cha sheria.

Majaji hao wamesema haikuwa sahihi kwa Fraser kubatilisha uamuzi uliotolewa na Bodi ya Ushauri ya Parole ya Matibabu kwamba Zuma atumikie kifungo chake nyumbani, lakini siyo kumwachia huru.

Kutokana na msimamo huo wa majaji, upo uwezekano mkubwa Zuma akarejeshwa gerezeni wakati wowote ambako alihukumiwa baada ya madai ya kukaidi na kudharau wito wa Mahakama ya Kikatiba ya Afrika Kusini.

Hata hivyo, idara za usalama za nchi hiyo yenye uchumi imara zaidi Afrika, zinahofia kuzuka kwa ghasia kama za awali ilipoamuriwa Zuma akatumukie kifungo cha miezi 15 kwa kosa hilo.

Miji mingi ya Afrika Kusini, ilikumbwa na ghasia na vurugu vilivyosababisha vifo na uharibifu mkubwa wa mali baada ya wafuasi wake kupinga hukumu hiyo na kumzuia kutoitekeleza.

Baada ya uamuzi huo wa mahakama ya juu, Fraser aliiambiwa televisheni ya SABC kwamba uamuzi wa kumwachia huru Zuma ulibebwa zaidi na ubinadamu na kwamba ulifanywa na yeye binafsi.

Wakati wa kutoa uamuzi wako, majaji watatu walihoji endapo Zuma baada ya kuachiwa ilihesabika anatumikia kifungo chake akiwa nyumbani au ilikuwa kwamba hukumu yake ilifutwa?

Baada ya kuachiwa Zuma (80) amekuwa akiishi kijijini kwake Nkandla na kwamba huenda maeneo ya mijini kwa nadra sana, hasa anapokwenda hospitali, Johannesburg au Pretoria.



Jacob Zuma

Zuma alianza kutumikia adhabu yake Julai 7, 2021 lakini alidumu gerezeni kwa takribani miezi miwili kabla ya kuachiwa huru na Fraser.

Inaonekana kwamba kamishna mpya wa Magereza, Makgothi Thobakgale, anaweza kumwita Zuma kuendelea na kifungo chake au ikaamuriwa vinginevyo.

Zipo taarifa kwamba mawakili wa Zuma wamejipanga kupinga amri ya kutakia kurejea gerezeni wakieleza kwamba aliachiwa kisheria.

Pamoja na mawakili hao kujipanga kumtetea, zipo taarifa kwamba chama cha DA, chenye wanachama na wafuasi wengi wazungu huenda kikaenda mahakamani hivi karibuni ikiwa Zuma hataitwa kuendelea na hukumu yake.

Zuma, ambaye alikuwa mwanaharakati aliyepinga ubaguzi wa rangi nchini kwake, alichaguliwa kuwa Rais wa Afrika Kusini May 2009 na kutumikia nafasi hiyo kwa miaka 9, kabla ya kuondolewa kwa kashfa ya kujihusisha na rushwa, matumizi manbaya ya madaraka na tuhuma zingine nyingi.

Mail & Guardian

Asili ya Banyamulenge wa Kitutsi DRC - II**Na Mwandishi WETU**

WIKI iliyopita katika kuichambua historia ya Banyamulenge walioko DRC, tulibaini kuwa asili yao inatoka katika mataifa mawili; Rwanda na Burundi na leo tunaendelea tulipoishia.

Serikali ya kikoloni ya Ubelgiji huko Kongo, ilitangaza kuwatambua Banyamulenge mnamo mwaka 1924. Iliwatambua kama wafugaji na kupewa nyanda kubwa ya Kivu kwa kuishi na kulisha mifugo.

Jambo hii liliwafanya kujiimarisha zaidi na kuwa na himaya kubwa ukanda wa mashariki mwa Kongo.

Aidha, kutambuliwa huko kuliwafanya kuingizwa kwenye sarafu ya noti ya faranga 10 ya Kongo ya kipindi cha ukoloni wa Wabelgiji.

Noti hiyo ilionyesha picha ya Watutsi wa Banyamrenge wakicheza ngoma ya Intore.

Baada ya uhuru wa Kongo mwaka 1960, serikali ya Kasavubu na baadaye ile ya Mobutu ilikataa kuwatambua Banyamulenge kama moja ya makabila ya Kongo, walionwa kama wakimbizi hivyo walitakiwa kurejea kwao Rwanda, Uganda na Burundi.

Hatua hiyo ikafanya Banyamulenge wengi kujiunga na “Uasi wa Simba” wa mwaka 1964-65, uasi huu ulikuwa ukiungwa mkono serikali ya Patrice Lumumba na waliongozwa na Anttone Kizenga.

Kufuatia hatua hiyo, jeshi chini ya Mobutu Seseseko ilipogundua uhusika wa Banyamulenge kuwasaidia waasi wa Simba, jeshi la Mobutu lilivamia kwenye makazi ya Banyamulenge na kuua ng’ombe pamoja na kuchoma vyakula chote.

Watutsi hao kuona hivyo, wakaamua kumuunga mkono Mobutu na kisha kupewa silaha kutoka kwa wanajeshi wanaomuunga mkono Mobutu na kusaidia kupambana na waasi. Baada ya vita hivyo kumalizika, Mobutu aliwahaidi

**Rais Laurent Kabila**

kuwatambua, lakini hakufanya hivyo kwa miongo kadhaa.

Banyamulenge waliendelea kujipanua eneo lote la mashariki ya Kongo, wengi wao walihamia kusini kuelekea eneo la Moba na Kalemi, ambapo kwa sasa ni Jimbo la Tanganyika, wakati wengine walihamia kwenye uwanda wa Ruzizi, ambapo huko wakatwaa ardhi kubwa yenye rutuba na kuwa machifu eneo hilo.

Huko walichanganyikana na Warundi na kufuga ng’ombe na walijishugulisha na kazi ya uuzaji wa nyama na maziwa, wafugaji hawa walienea ndani ya wilaya tatu za Mwenga, inayokaliwa na watu wa Lega, Fizi inayokaliwa na watu wa Bembe, na Uvira, inayokaliwa na watu wa makabila ya Vira, Bafuliro, Wabwale

Asili ya Banyamulenge wa Kitutsi DRC - II

Inatoka Uk. 20

na Wa-Barundi.

Mvutano wa kikabila dhidi ya Watutsi wa Kinyamulenge na serikali ya Mobutu ulizidi kuongezeka kufuatia mauaji ya halaiki ya Wahutu nchini Burundi ya mwaka 1972, hatua hiyo ilisababisha Banyamulenge kuanza kudai vitambulisho vya wakaazi wa Mulenge na kutambuliwa kama raia wa Kongo (DRC).

Hali hii ilichochea mvutano wa kisiasa wa mwaka 1971-1992 baada ya kupitiswa sheria ya uraia ya mwaka 1971. Hapo ukaibuka mgogoro wa mwaka 1993-1998 kufuatia sheria iliyowaruhusu kupiga kura, lakini ikawazuia kuwania nafasi yoyote ile ya uongozi wa kisiasa.

“Mkataba wa Lemela” ni mkataba ulioandaliwa na mataifa ya magharibi kufadhili vikosi vya waasi wa kabila la Banyamulenge ambao ndio chanzo cha ajenda ya kuiondoa serikali ya Mobutu na kuigawa Kongo DRC ili Banyamulenge wapate nchi mashariki mwa Kongo.

Lakin pia kumekuwepo na dhana nyingine inayozihusudu Rwanda na Uganda juu ya hiki kinachoitwa “Mkataba wa Lemela”

Kwa mfano, inadaiwa kuwa kikosi cha waasi wa M23 kinafanya kazi kwa maelekezo ya serikali ya Rwanda na kimefanikiwa kwa kiasi kuinua uchumi wa Rwanda kwa kudhibiti maeneo kadhaa ya machimbo ya madini.

Baada ya miaka miwili ya urais, Rais Laurent Desire Kabila alitangaza kuwa wageni wote waandoke nchini Kongo aliongeza kwa kufafanua, kwamba Wanyarwanda na Wanyamulenge warudi kwao na kusema anawashukuru kwa kazi waliyofanya wakati wa mapambano ya kumuungiza Ikulu.

Rais Kabila alinukuliwa akisema kuwa Makubaliano ya Lemela ni “makubaliano ya porini” na kwamba yeye hakuwa na madaraka ya kuuza nchi. Alisema hakatai kuwepo mkataba, lakini akataka hilo lipelekwe kwa wananchi kupitia bunge ili wananchi wenyewe waamue.

Hata hivyo, Kabila aliuawa kabla

hajamaliza kunyukana na Banyamulenge na nafasi yake kuchukuliwa na mtoto wake, Joseph Kabila.

Vita ya M23 ilipoanza Wanyamulenge wengi waliunga mkono na kujiunga na kikundi hicho kilichoongozwa na Kundabatware mtutsi wa Kutoka Kivu kaskazini.

Vuguvugu la waasi la M-23, liliungwa mkono na Rwanda, Licha ya kwamba wengi wa Banyamulenge walipinga uungwaji mkono wa Rwanda huku wakitaka vuguvugu hilo kutambulika kama vita ya Banyamulenge ndani ya Kongo inayoongozwa na Banyamulenge.

Kupitia M23 hawakufanikiwa kwa kuwa vuguvugu hilo lililibebe sura ya ujasusi wa Rwanda nchini Kongo, hivyo Banyamulenge wakawa wameshindwa, japo waliendeleza madai yao yenye matakwa matatu;

Moja, wanahitaji kupatiwa jimbo la kiutawala katika ene la mashariki mwa Kongo, yaani jimbo la Kivu Kusini na Kaskazini yagawanywe na kupatikana jimbo lao ambapo jiji la Uvira ndio iwe makao makuu ya jimbo lao.

Pili, kutambuliwa kwenye sheria zote na kupewa haki bila kuwepo kwa kizuizi chochote.

Tatu, ikiwa yote yatashindikana, basi eneo la mashariki mwa Kongo ligawanywe ili wao wapate nchi yao, yaani nchi ya asili ya mababu zao.

Madai yote hayo serikali ya Joseph Kabila iliyapuuza mwaka 2013 ilipoigawa upya nchi katika majimbo mapya.

Kabila aliwapatia wilaya iliyoitwa Minembwe huko Kivu Kusini, na kukubali dai lao la pili japo sheria ya uraia iliyofanyiwa mabadiliko mwaka 2012 haikuwapa haki zote za uraia.

Mpaka sasa kuna idadi kubwa ya Banyamulenge wanaoishi Rwanda kama wakimbizi kutoka Kongo na wengine ni raia wa Rwanda wanaofaidika na ulinzi wa serikali inayoongozwa na Watutsi nchini Rwanda.

Itaendelea sehemu ya mwisho wiki ijayo

Katiba, serikali na uhuru binafsi

Na Deusdedith KAHANGWA

KATIBA ya kidemokrasia inapaswa kusaidia jamii kuepuka matatizo mawili ya kiutawala; mosi, ni “dola inayoongozwa na serikali ya holela,” yaani “leisefair state.” Na pili, ni “dola inayoongozwa na serikali ya mabavu,” yaani “totalitarian state.”

Kanuni kwamba, kila mtu na kila kikundi, humiliki “boma la utawala binafsi,” ambamo serikali itaingia ili kutoa msaada wa mpito kwa mwenye boma aliyelemewa.

Mwanafalsafa Profesa John Mitchell Finnis (82), mzaliwa wa Australia, ametoa mwongozo wa kujenga mipaka ya “boma la utawala binafsi.” Rejea kitabu chake, “Natural Law and Natural Rights (2011),” ukurasa wa 199 hadi 200.

Profesa Finnis anasema kuwa, Katiba ya nchi inayoheshimu misingi ya utawala bora, inapaswa kutambua aina sita za haki.


Kuna haki zinazohusu madai chanya, madai hasi, uhuru chanya, uhuru hasi, kibali cha kubadilisha haki za watu baki, na haki zinazohusu kizuizi cha kubadilisha haki za watu baki.

Mosi, kuhusu madai chanya, mtu mmoja atakuwa na haki ya kudai kwamba mtu baki atekeleze kitendo fulani, endapo kuna kanuni bayana inayotamka kwamba mtu baki analo jukumu la kutekeleza kitendo hicho (positive claim right).

Pili, kuhusu madai hasi, mtu mmoja atakuwa haki ya kudai kwamba mtu baki asitekeleze kitendo fulani, endapo kuna kanuni bayana inayotamka kwamba mtu baki analo jukumu la kujizuia kutekeleza kitendo hicho (negative claim right).

Tatu, kuhusu uhuru chanya, mtu mmoja atakuwa na haki ya uhuru wa kufanya kitendo fulani, endapo hakuna kanuni bayana inayotamka kwamba mtu huyo ana jukumu la kujizuia kutekeleza kitendo hicho kwa faida ya mtu baki (positive liberty right).

Nne, kuhusu uhuru hasi, mtu mmoja



Prof. Finnis

atakuwa na haki ya uhuru wa kutofanya kitendo fulani, endapo hakuna kanuni bayana inayotamka kwamba mtu huyo ana jukumu la kutekeleza kitendo hicho kwa faida ya mtu baki (negative liberty right).

Tano, kuhusu kibali cha kubadilisha haki za watu baki, mtu mmoja atakuwa na haki ya kubadilisha au kusitisha haki za mtu baki, endapo kuna kanuni bayana inayotamka kwamba haki za mtu baki, zinaweza kubadilishwa au kusitishwa na mtu huyo (power right).

Na sita, kuhusu kizuizi cha kubadilisha haki za watu baki, mtu mmoja atakuwa na kinga dhidi ya haki zake kubadilishwa na mtu baki, endapo kuna kanuni bayana inayomzuia mtu baki kubadilisha au kusitisha haki za mtu huyo (immunity right).

Kwa mujibu wa Profesa Finnis, basi, serikali isiyotambua mipaka tajwa ya “boma la utawala binafsi,” ama ni “serikali ya kiimla” au ni “serikali ya holela.”

Mashabiki Afrika wahuisha matumaini



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Ghana

Na Mwandishi WETU

USHINDI wa Timu ya Taifa ya Morocco dhidi ya Ubelgiji jana umeendelea kuuhisha matumaini ya timu za Afrika katika michuano ya Soka Kombe la Dunia, baada ya kuungana na Senegal kupata pointi tatu katika mechi ya pili.

Morocco iliishinda timu ngumu ya Ubelgiji kwa mabao 2-1, wakati Senegal ikiichakaza timu wenyeji Qatar kwa mabao 3-1.

Hata hivyo, pamoja na matumaini kufufuka, timu tano za Afrika ambazo zinashiriki michuano ya Kombe la Soka la Dunia nchini Qatar, zilianza kwa “miguu mibaya” ya kufungwa.

Cameroon, Senegal na Ghana, timu kubwa zilizokuwa zikiweka matumaini ya kulitoa kimasomaso bara hilo la Afrika, zilianza kwa kufungwa katika mechi zao zote za ufunguzi kwenye makundi yao.

Wakati Ghana ikifungwa 3-2 dhidi ya Ureno, Cameroon walipoteza mchezo wao dhidi ya Uswisi huku Senegal wakifungwa kizembe 2-0 na timu ya Uholanzi. Baadaye, Morocco na Tunisia zikatoka sare dhidi ya Croatia na Denmark mtawaliwa

Timu tatu za Afrika; Cameroon, Senegal na Ghana zilizokuwa zikipewa nafasi ya kufanya maajabu katika kombe hilo kwa mwaka huu, zilishindwa kufanya ilivyotarajiwa na badala yake zote zilifungwa na wapinzani wao katika

mechi zao za ufunguzi.

Timu za Afrika sasa zinahitaji kufanya kazi ya ziada kuweza kusonga mbele na hatimaye kupata mwanya wa kufanya vyema zaidi kwenye hatua za mtoano.

Tayari Senegal imeshinda mechi yake ya pili dhidi ya Timu ya Taifa ya Qatar kwa kuichakazi mabao 3-1 Jumaat iliyopita. Na pia jana kwa Morocco kuichabanga Ubelgiji kwa jumla ya mabao 2-0.

Endapo timu zingine za Afrika zitapoteza michezo za pili, uwezekano wa kuendelea utafifa, hivyo kuzinyima – kwa mara nyingine tena, nafasi ya kufika robo fainali na kuliheshimisha bara la Afrika lenye wachezaji lukuki wanaochezea timu za mataifa mengine zinazowafunga ndugu zao.

Idadi kubwa ya mashabiki jijini Dar es Salaam wanasikika wakieleze kusikitishwa kwao na matokeo yaliyopatikana kwa timu za Afrika.

“Kama hakuna mabadiliko katika mfumo wa uchezaji, ndoto ya miaka mingi ya angalau Afrika kuwa na timu inayotinga nusu fainali za Kombe la Dunia, itaendelea kututafuna kila michuano hiyo inapowadia,” analalamika Michah Ochieng’ – shabiki anayehusudu Senegal.

Shabiki mwingine, Mariam Kashinde, aliyejitambulisha kwa Pambazuko kuwa ni shabiki wa Ghana, amelalamika kiwango kisichoridhisha cha timu yake katika mechi ya ufunguzi dhidi ya Ureno, Novemba 24.

PAMBAZUKO KUSHABIKIA GHANA



Mmoja wa mashabiki wa Timu ya Taifa ya Soka ya Ghana (Black Stars) aliyeko Accra, Ghana, hakukata tamaa licha ya timu yake kufungwa 3-2 dhidi ya Ureno katika mchezo wa Novemba 24. Ghana licha ya kuonyesha kiwango cha juu cha mpira, lakini ilipoteza, hata hivyo bado ina nafasi ya kuendelea endapo itapata pointi tatu dhidi ya Timu ya Jamhuri ya Korea - Jumatatu, Novemba 28. Pambazuko limetangaza rasmi kwamba linashabikia timu hiyo na litatoa ushirikiano kwa kila linalowezekana ili timu hiyo ishinde. (Picha kutoka © Misper Apawu/AP)

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.